## Mambo yatakayowasilishwa na *GroFutures* ni pamoja na:

### Maarifa mapya & takwimu tokana

- Uelewa wa kiasi cha mikondo ya maji chini ya ardhi
- Uboreshaji wa makadirio ya uhifadhi wa maji chini ya ardhi na mzunguko wake
- Kuunganisha pamoja uangalizi wa viwango vya mikondo ya maji chini ya ardhi barani Afrika ili kutathmini mahusiano ya tabia nchi na maji chini ya ardhi
- Ufuatiliaji wa data zinazojirudia sana katika kutathmini mchakato wa kuongeza maji na mwingiliano wa maji chini ya ardhi - maji kwenye uso wa ardhi
- Ukadiriaji wa kiasi cha ongezeko la maji chini ya ardhi na uhifadhi kwa kutumia makadirio ya mabadiliko ya hali ya hewa na matumizi ya ardhi kwa shughuli za binadamu



*Uthibiti wa kina cha maji ya ardhini Tanzania*

### Vifaa vipya na mahusiano

- Uimarishaji wa uwezo na ushirikiano wa utafiti katika Afrika
- Mtandao wa kuangalia maji chini ya ardhi barani Afrika
- Vituo vya maji chini ya ardhi kusaidia watoa maamuzi kutathmini maoni ya wasio na mamlaka ya kuhusishwa na michakato ya maendeleo
- Uundaji wa mfumo ili kuwezesha usimamizi wa pamoja wa maji yaliyo chini ya ardhi
- Modeli inayoonyesha ongezeko na uhifadhi wa maji chini ya ardhi zitakazotathimini uendelevu wa matumizi ya maji chini ya ardhi na mfumo wa ikolojia unaotegemea maji ya ardhini

## Ubia/Wahisani wa *GroFutures*:

UCL
IRD Institut de recherche pour le développement
igrac International Groundwater Resources Assessment Centre
WITS University
IDS Institute of Development Studies
STEPS centre
IWMI International Water Management Institute
British Geological Survey Natural Environment Research Council
University of Sussex

Chuo Kikuu cha Addis Ababa (AAU), Ethiopia
Watafiti wa Miamba wa Uingereza (BGS), Uingereza
Taasisi ya Taaluma za Maendeleo (IRD), Ufaransa
Taasisi ya Taaluma za Maendeleo (IDS), Uingereza
Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti/kutathimini Rasilimali Maji Ardhini (IGRAC)
Taasisi ya Kimataifa ya Usimamizi wa Maji (IWMI)
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Tanzania
Chuo Kikuu cha Abdou Moumouni de Niamey (UAM), Niger
Chuo Kikuu cha Ngaoundéré (UN), Kameruni
Chuo Kikuu cha London (UCL), Uingereza
Chuo Kikuu cha Maiduguri (UM), Nigeria
Chuo Kikuu cha Sussex (UoS), Uingereza
Chuo Kikuu cha Witwatersand (Wits), Afrika Kusini

## Washirika wa *GroFutures*:

- Wizara ya Maji, Nishati na Umwagiliaji (Ethiopia)
- Mamlaka ya Bonde la Awash (Ethiopia)
- Wakala wa Mabadiliko katika Kilimo (Ethiopia)
- Wizara ya Maji na Mazingira (Niger)
- Mamlaka ya Bonde la Niger
- Wizara ya Maji (Tanzania)
- Bodi ya Maji ya Bonde la mto Rufiji (Tanzania)
- Mtandao wa Maji ya Ardhini Afrika (AGW-Net)

UKaid from the British people
UPGro Unlocking the Potential of Groundwater for the poor
upgro.org
NERC 50 Science of the Environment
ESRC Economic & Social Research Council

**email:** contact@grofutures.org
**web:** www.grofutures.org

# GroFutures



## Hali ya maji ya chini ya ardhi katika Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara



***Kukuza msingi, taratibu na usimamizi shirikishi kwa njia za kisayansi ambazo rasilimali za maji chini ya ardhi zinaweza kutumika kwa uendelevu kupunguza umaskini katika Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara***

***(2015 - 2019)***

**www.grofutures.org**

**Maji** yaliyo chini ya ardhi ni chanzo muhimu cha maji safi na salama ya kunywa, kufanya usafi, umwagiliaji na uendeshaji sekta ya viwanda Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara. Maji ya chini ya ardhi pia huhimili mito, maziwa na maeneo oevu wakati mvua inapokuwa chini ya wastani au haipo kabisa.



*Kukusanya maji ya chemichemi huko Kampala, Uganda*

## *GroFutures* inalenga katika:

- Kupunguza kutokuwa na uhakika katika vyanzo vinavyoweza kujirudia na wingi wa upatikanaji maji chini ya ardhi ili kukidhi mahitaji ya baadaye kwa ajili ya chakula, maji na huduma za kimazingira
- Kukuza ushirikishwaji wa sauti za watu maskini katika utoaji wa maamuzi juu ya maji ya chini ya ardhi kwa maendeleo yao
- Kuimairisha utegemezi wa maji ya chini ya ardhi kwa mahitaji ya kuongeza upatikanaji wa chakula na maji na kuwepo kwa tofauti za mvua na utiririkaji wa mito utokanao na mabadiliko ya tabia nchi



*Kisima cha jangwani katika eneo la kati la Tanzania (jangwa)*

## Jopo la kimataifa:

*GroFutures* imekusanya wanajopo wataalam mashuhuri wa kimataifa kutoka Afrika na Ulaya kuhusiana na sayansi ya usimamizi na utawala wa maji ya ardhini.



*Wajumbe wa GroFutures mjini London*

## Mtandao wa Kiafrika wa watafiti na watu wanaoshughulika na maji ya ardhini (NAGO):

*GroFutures* itaanzisha mtandao wa watafiti na watu watakaoshughulikia maeneo nyeti na muhimu kwa mazingira katika uhifadhi wa maji yaliyo chini ya ardhi na changamoto za usimamizi wake katika Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara. Shughuli za utafiti zitaelekezwa zaidi katika mabonde ya mito nchini Ethiopia, Niger na Tanzania.




## Ushirikishwaji katika Usimamizi wa maji ya chini ya ardhi:

*GroFutures* itaendeleza umoja na mfumo shirikishi katika usimamizi wa maji yaliyo chini ya ardhi ambapo maoni ya wanawake na wanaume maskini yatazingatiwa pamoja na wale wasio na mlengo wowote ili kupanua maendeleo na matumizi ya chini ya ardhi.



*Wadau washiriki wa mkutano nchini Kenya*

## Uendelevu wa maji yaliyo chini ya ardhi:

*GroFutures* itatumia mbinu mpya ya Jiofizikia na kukusanya pamoja maoni ya muda mrefu ya viwango vya maji yaliyo chini ya ardhi kwa kiasi kikubwa kuboresha ujuzi wa vyanzo vinavyojirudia na kiasi cha maji yaliyo chini ya ardhi katika Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara.



*Kukadiria uhifadhi maji chini ya ardhi kwa kutumia Jiofizikia nchini Burkina Faso*